

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SERA YA MALIKALE

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

DAR ES SALAAM
2008

Ni imani ya Serikali kuwa utekelezaji wa Sera hii utasaidia kuboresha uhifadhi endelevu wa malikale, kuongeza kiwango cha uelewa wa malikale kwa wananchi, kuwaongezea wananchi hali ya kujiamini na kujivunia utaifa wao.

© Haki miliki 2008: Idara ya Mambo ya Kale
S. L. P. 2280
Dar es Salaam.

ISBN: 9987 - 440 - 05 - 3

YALIYOMO

YALIYOMO..... ii
VIFUPISHO..... iv
DIBAJI..... v
FAHARASA..... viii
SURA YA KWANZA..... 1
1.0 UTANGULIZI..... 1
1.1 Dhana ya Malikale..... 1
1.2 Malikale na Maendeleo..... 1
1.3 Malikale na Elimu..... 2
1.4 Malikale na Teknolojia..... 2
1.5 Malikale na Utalii..... 2
1.6 Malikale na Utambulisho wa Taifa..... 3
1.7 Malikale na Utamaduni..... 3
1.8 Malikale na Burudani..... 4
1.9 Malikale na Mazingira..... 4
SURA YA PILI..... 5
2.0 HALI HALISI YA MALIKALE..... 5
2.1 Utafiti wa Malikale..... 5
2.2 Uhifadhi wa Malikale..... 6
SURA YA TATU..... 10
3.0 UMUHIMU NA MALENGO YA SERA..... 10
3.1 Umuhimu wa Sera ya Malikale..... 10
3.2 Malengo ya Sera ya Malikale..... 10
SURA YA NNE..... 12
4.0 HOJA NA MATAMKO YA SERA..... 12
4.1 Utafiti..... 12
4.2 Uhifadhi..... 14
4.3 Kumbukumbu..... 17

4.4 Takwimu..... 19
4.5 Ushirikishwaji wa Wadau..... 20
4.6 Uwekezaji katika Utalii wa Utamaduni..... 22
4.7 Utaalamu, Mafunzo na Ajira..... 23
4.8 Vitendea Kazi..... 25
4.9 Maeneo ya Malikale..... 26
4.10 Ushirikiano wa Kimataifa..... 28
SURA YA TANO..... 30
5.0 MASUALA MTAMBUKA YA SERA..... 30
5.1 Serikali Kuu..... 30
5.2 Serikali za Mitaa..... 31
5.3 Jamii..... 32
5.4 Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali..... 32
5.5 Sekta Binafsi..... 33
5.6 Jumuiya za Kikanda na Kimataifa..... 34
5.7 Mawakala wa Serikali na Vyombo vingine vya Dola..... 3 4
SURA YA SITA..... 35
6.0 MUUNDO WA KITAASISI NA KISHERIA..... 35
6.1 Muundo wa Kitaasisi..... 35
6.2 Muundo wa Kisheria..... 35
SURA YA SABA..... 37
7.0 MWISHO..... 37

VIFUPISHO

BAKITA: Baraza la Kiswahili Tanzania

BASATA: Baraza la Sanaa Tanzania

ICCROM: International Centre for the Study of the Preservation and Restoration of Cultural Property (Kituo cha Kimataifa cha Mafunzo ya Uhifadhi na Ukarabati wa Mali za Kiutamaduni).

ICMAH: International Committee on the Management of the Archaeological Heritage (Kamati ya Kimataifa ya Uendeshaji wa Urithi wa Kiakiolojia).

ICOM: International Council for Museums (Baraza la Kimataifa la Makumbusho).

ICOMOS: International Council on Monuments and Sites (Baraza la Kimataifa la Maeneo na Majengo ya Kihistoria).

UNESCO: United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni)

DIBAJI

Suala la kutambua maana na umuhimu wa malikale kwa jamii siyo jambo geni kwa Watanzania. Tangu enzi za wahenga wetu, kabla Wazungu hawajaingilia uendeshaji wa utawala na utamaduni wa jamii zetu, wakazi wa Tanzania na kwingineko duniani walikuwa wanaenzi na kuhifadhi vitu vya kale vilivyokuwa vimejipatia umuhimu fulani kutokana na mchango wake katika jamii husika. Mathalani, sehemu zilizotumika kwa kuabudia na kutolea matambiko kama vile misitu, mapango, maporomoko ya mito na maeneo mengine ambayo jamii iliyaona kuwa yana umuhimu wa pekee, yalitunzwa vizuri sana na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Isitoshe, siyo kila mtu aliruhusiwa kuzifikia sehemu hizo, bali watu au koo chache zilizokubaliwa na jamii kwa misingi ya kihistoria ya jamii hizo. Kulitokea pia sababu zilizowafanya watu binafsi au makundi ya watu wahifadhi zana au silaha kama vile mikuki, mashoka, majembe au mavazi na kuvirithisha vitu hivyo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mara nyingi vitu hivi vilikuwa ni vile ambavyo vilisaidia kwa namna fulani kuokoa maisha ya mhusika, ama tu vilitumika na mtu maarufu katika jamii na ndugu zake wa karibu walipenda kuvihifadhi ili viendelee kuwakumbusha juu ya mtumiaji huyo.

Madhumuni ya uhifadhi wa malikale ya wakati huo hayana tofauti na yale ya leo. Kinachobadilika hasa ni mbinu ambazo zinaendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Shughuli za uhifadhi wa kisasa wa malikale nchini zilianza rasmi mwaka 1937 ilipoundwa Sheria ya Uhifadhi wa majengo ya Kihistoria. Tangu kipindi hicho, na hata baada ya kuanzishwa idara ya Mambo ya Kale mwaka 1957 ikiwa ni

chombo cha kusimamia uhifadhi wa malikale, uendeshaji wa shughuli za sekta ya malikale umetegemea sera za Utalii na Utamaduni pamoja na kanuni na Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na marekebisho ya mwaka 1979. Uzoefu umeonesha kwamba sheria inayosimamia malikale imekuwa na upungufu kwa kutokuwepo na Sera ya Malikale. Kwa maneno mengine, sera ndiyo inayosimamia na kuongoza sheria na siyo vinginevyo.

Imebainika kuwa jinsi muda unavyopita, kasi ya mabadiliko ya teknolojia, uchumi, jamii, siasa na mazingira inaongezeka sana. Mabadiliko haya yanaweza kuyumbisha uendeshaji wa taasisi kama hakuna dira madhubuti inayotoa msimamo wa uelekeo wa namna ya kukabiliana nayo. Kwa mantiki hii, Wizara ya Maliasili na Utalii, imeamua kuandaa SERA YA MALIKALE. Lengo la sera hii ni kufafanua dhima na malengo ya malikale, kuainisha jinsi shughuli za malikale zitakavyoendeshwa na kusimamiwa, kusisitiza umuhimu wa kutafiti na kuhifadhi malikale pamoja na kufafanua jinsi wadau mbalimbali ikiwamo serikali na taasisi zake, sekta binafsi na umma kiujumla watakavyoshirikishwa katika shughuli za uhifadhi wa malikale.

Katika utekelezaji, sera hii imetoa kipaumbele katika ushirikishwaji wa umma ambao ndio mmiliki mkuu wa rasilimali hii muhimu. Ni nia ya serikali kuona kuwa utafiti, uhifadhi, ulinzi na uendeshaji wa malikale unashughulikiwa na wananchi kwa karibu zaidi kuliko ambavyo imefanyika hadi sasa. Dhima ya serikali itakuwa kuandaa mazingira mazuri yatakayoliwezesha jambo hilo kutekelezwa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wake.

Ni imani ya serikali kuwa utekelezwaji wa sera hii utasaidia

kuboresha uhifadhi endelevu wa malikale, kuongeza kiwango cha uelewa wa malikale kwa wananchi, kuwaongezea wananchi hali ya kujiamini na kujivunia utaifa wao, na kupanua wigo wa vitegauchumi kwa kuwekeza katika sekta ya utalii wa utamaduni na kuendesha makumbusho na maduka ya vitu vya utamaduni.

Mhe. Shamsa S. Mwangunga
WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII

FAHARASA

Asasi za malikale: Vyombo, hususan vyuo na shule vinavyotoa elimu na taaluma ya malikale.

Eneo la malikale: Mahali ambapo masalia ya kale au kumbukumbu muhimu za kihistoria zinapatikana.

Kumbukumbu: Taarifa za zamani au masalia yanayobaini urithi wa utamaduni.

Majengo ya kihistoria: Kumbukumbu yoyote ya majengo, kwa mfano nyumba, kaburi, au ngome yenye umri wa miaka mia moja au zaidi na ambayo yana umuhimu fulani kiutamaduni.

Malikale: Malikale hujumuisha rasilimali za utamaduni, zinazoshikika na zisizoshikika; zinazohamishika, na zisizohamishika zilizo nchi kavu na majini zenye umri wa miaka mia moja (100) na kuendelea, au zile ambazo zimeainishwa hivyo kulingana na kanuni na sheria za serikali zinazosimamia malikale nchini.

Mambo ya Kale: Dhana ambayo hadi sasa imekuwa ikitumika kuelezea rasilimali zilizoainishwa chini ya 'malikale', na kwayo zimepatikana dhana kama vile

'Idara ya Mambo ya Kale', 'Sheria ya Mambo ya Kale' na kadhalika. Lakini dhana hii haitoi uzito unaostahili juu ya rasilimali zenyewe kama ilivyo kwa dhana ya 'malikale'.

Matumbawe: Aina ya mawe mororo yapatikanayo baharini yenye madini ya chokaa yatokanayo na mkusanyiko mkubwa wa mifupa, magamba na makombe ya wanyama wadogo wa baharini.

Metali: Kitu chenye asili ya chuma.

Oldupai: Neno Oldupai lina asili ya lugha ya Kimaasai, likiwa na maana ya mmea wa katani-mwitu (Sansevieria ehrebergiana). Mmea huu unapatikana kwa wingi katika eneo lote la Korongo la Oldupai. Watafiti wa mwanzo walipotosha matamshi ya neno hili toka Oldupai na kuwa Olduvai bila kudhamiria. Kimila, Wamasai hutoa majina ya maeneo kwa kuoanisha na vitu vya asili vilivyopo katika maeneo husika. Kwa kuzingatia umuhimu wa eneo husika, jina la Oldupai linabeba dhana sahihi kwani linaelezea uasili na utamaduni wa Mtanzania.

Sera: Tamko linalotoa dira au mwelekeo wa kufanikisha tendo lililokusudiwa.

Takwimu: Hesabu au namba za kumbukumbu au za matukio. Mara nyingi hutumika katika kufanya tathmini ya jambo, mathalani kuongezeka au kupungua kwa tija katika taasisi.

Teknolojia ya jadi: Mbinu za asili za utengenezaji zana, silaha na vifaa vingine.

Teknolojia: Ubunifu, ustadi, mbinu na taratibu za kutengeneza vifaa mbalimbali vyenye kuweza kurahisisha maisha ya binadamu.

Tunu: Kitu cha thamani ambacho kimefichwa kwa siri chini ya ardhi ambacho upatikanaji wake unahusisha uchimbuzi.

Uhifadhi wa malikale: Utunzaji wa malikale kwa lengo la kuziwezesha zidumu kwa muda mrefu kuliko kama zingeachwa bila matunzo.

Uhifadhi endelevu: Utaratibu wa uhifadhi unaohakikisha kuwa kunakuwepo mipango na mbinu za kudumu za kutunza, kuendeleza na kuendesha malikale ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa muda mrefu. Mara nyingi utaratibu huu huhusisha wananchi waishio maeneo yenye malikale hizo. Wao huzihifadhi kama sehemu ya maisha yao ya kila siku.

Ukarabati wa malikale: Ni mchakato wa kurejesha sura, usanifu na ubunifu wa asili wa malikale zilizochakaa au kuharibika kutokana na shughuli za binadamu au nguvu za asili kama vile mvua, upepo na tetemeko la ardhi kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya uhifadhi.

Urithi wa utamaduni unaohamishika: Kumbukumbu za utamaduni zinazoweza kuchukuliwa na kubebwa kutoka sehemu moja hadi nyingine, kama vile zana, silaha, mavazi, na mapambo.

Urithi wa utamaduni unaoshikika: Kumbukumbu za utamaduni zenye umbile linalogusika kama vile maeneo ya malikale, majengo, zana na silaha.

Urithi wa utamaduni usiohamishika: Kumbukumbu za utamaduni zisizowezekana kuchukulika wala kubebeka kutoka sehemu moja hadi nyingine, kama vile maeneo ya malikale, majengo na mapango.

Urithi wa utamaduni usioshikika: Kumbukumbu za utamaduni zisizokuwa na umbile linalogusika kama vile lugha, sanaa za lugha, maigizo, imani, mila, simulizi na desturi.

Urithi wa utamaduni: Kumbukumbu zote za utamaduni, zinazoshikika na zisizoshikika, ikiwa ni pamoja na masalia ya maumbile yake, wanyama na mimea aliyotumia binadamu kwa ajili ya chakula na ujenzi, maeneo yanayobaini shughuli alizozifanya, zana mbalimbali alizotumia, lugha, misemo, imani, mila na desturi.

Ushirikishwaji wa umma: Kuwapatia wananchi fursa katika kupanga na kutekeleza mipango ya uhifadhi wa malikale zilizopo katika maeneo yao.

Visukuku: Mabaki ya kale ya miili ya viumbe au alama zilizoachwa na viumbe hao zikithibitisha kwamba waliishi hapo kale.

Wadau wa malikale: Serikali, taasisi, mashirika, vikundi na watu binafsi wanaojihusisha kwa namna mbalimbali na malikale.

Zamadamu: Familiasafu ya wanyama waliotembea kwa miguu miwili kama binadamu lakini walikuwa na maumbile duni kama masokwe na uwezo mdogo wa kufikiri, walioishi Afrika miaka zaidi ya milioni moja iliyopita.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Dhana ya Malikale

Malikale hujumuisha rasilimali za utamaduni, zinazoshikika na zisizoshikika; zinazohamishika, na zisizohamishika zilizo nchi kavu na majini zenye umri wa miaka mia moja (100) na kuendelea, au zile ambazo kutokana na umuhimu wake zimeainishwa na kutangazwa na Waziri mwenye dhamana kulingana na kanuni na sheria za serikali zinazosimamia malikale nchini. Rasilimali hizo zinadhihirisha historia na mabadiliko ya kimaumbile na ya kiutamaduni ya binadamu kuanzia chimbuko lake hadi leo. Rasilimali hizo ni pamoja na masalia ya zana za mawe, metali, miti na mifupa; visukuku vya binadamu, mimea na wanyama; michoro ya miambani; magofu kama vile makaburi, nyumba na ngome za kujilinda; maeneo ya matambiko kama vile mapango, misitu, miti, vichaka, mito, milima na mimea iliyoteuliwa na jamii za kale kwa madhumuni ya ibada na kumbukumbu za matukio muhimu ya kihistoria, yakiwemo ya viongozi na mashujaa. Tanzania inayo hazina kubwa ya malikale yenye kubaini vipengele vyote vilivyotajwa hapa.

1.2 Malikale na Maendeleo

Malikale inatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya wananchi na serikali kwa ujumla. Mchango huo unaweza kuwepo katika nyanja za utalii, uchumi, teknolojia, utafiti na elimu. Umuhimu huu ndio unaojenga hoja ya uhifadhi wa rasilimali hii. Uhifadhi huzilinda malikale dhidi ya uharibifu wa aina yoyote na hivyo kudumisha umuhimu na thamani

yake. Kamwe, uhifadhi haulengi katika kuzuia maendeleo bali huongeza kasi ya maendeleo yaliyoratibiwa. Hii ni kwa sababu matumizi ya malikale yakiachiwa holela yanaweza kuchangia katika kuharibu na kupotea kwa amali hiyo.

1.3 Malikale na Elimu

Malikale ni moja kati ya nyenzo muhimu katika kuwaelimisha watu juu ya historia na utamaduni wao. Hayo hufanyika kwa kuwawezesha watu kuona vitu halisi vitokanavyo na urithi wa utamaduni. Zaidi ya hayo, malikale huwawezesha watu kutambua na kuthamini utu wao, historia yao na utamaduni wao.

1.4 Malikale na Teknolojia

Malikale nyingi zimetengenezwa na binadamu, na kwa maana hiyo ni mazao ya teknolojia. Kwa hiyo zinapohifadhiwa husaidia kuthibitisha na kuonesha chimbuko la teknolojia na ustaarabu wa binadamu. Teknolojia za jadi zikifahamika kwa watu wenye vipaji na ubunifu zinaweza kuboreshwa sambamba na zile za kisasa na hivyo kupanua wigo wa uwezo wetu wa kuyatawala na kuyatumia mazingira kwa njia endelevu.

1.5 Malikale na Utalii

Malikale ni kitegauchumi muhimu sana kwani ni kivutio kizuri cha watalii. Nchi nyingi duniani hupata mapato makubwa kutokana na utalii unaotegemea vivutio vya malikale. Utalii huchangia na kuongeza pato la serikali na la wananchi wanapofanyakazi katika sekta hiyo ama wanapouza bidhaa na huduma mbalimbali kwa watalii. Kuna uwezekano pia wa

kuuza vitu vya utamaduni ama nakala za malikale kwa kufuata utaratibu wa kisheria na hivyo kujipatia kipato na kupunguza umaskini.

1.6 Malikale na Utambulisho wa Taifa

Malikale ni kitambulisho cha taifa husika. Tanzania inazo kumbukumbu nyingi muhimu zenye sifa za kimataifa. Baadhi yake zimeishaitangaza nchi yetu nje ya mipaka yake. Mifano halisi ni pamoja na fuvu la zamadamu aliyeishi miaka milioni 1.75 iliyopita lililogunduliwa mwaka 1959 katika Bonde la Oldupai, na nyayo za zamadamu aliyeishi miaka milioni 3.6 iliyopita katika eneo la Laetoli, nyayo ambazo ni upendeleo wa Tanzania pekee kwani ushahidi wa aina hii haujapatikana mahali pengine popote duniani.

Licha ya uwingi na ubora, michoro ya miambani iliyopo Tanzania ina umri unaokadiriwa kuwa mkubwa kuliko sehemu nyingine duniani kote na ina mitindo mbalimbali inayodhihirisha uwezo na umahiri wa hali ya juu wa wahenga wetu unaolitambulisha taifa na kulitofautisha na mataifa mengine. Pia katika ukanda wa mwambao, hususan katika maeneo ya Kilwa, Kunduchi, Kaole, na Tongoni kuna utajiri mkubwa wa magofu ya majengo ya matumbawe yanayobaini uhusiano wetu wa kibiashara na kiutamaduni na mataifa ya mabara ya Asia na Ulaya kuanzia karne nyingi zilizopita. Pia Tanzania ina bahati ya kuwa na makabila ya kijamii zaidi ya 120, na kila moja lina lugha yake, na hivyo kuiongezea nchi hii utajiri wa utamaduni na utambulisho wa Taifa.

1.7 Malikale na Utamaduni

Malikale ni kielelezo cha utamaduni na ustaarabu wa jamii

katika hatua mbalimbali za maisha. Huionesha na kuikumbusha jamii husika chimbuko la tabia, mila na desturi ambazo inazitumia iwe katika uwanja wa uchumi, siasa, teknolojia, elimu na kadhalika. Jamii yoyote ile inatambuliwa na kuthaminiwa kutokana na utamaduni wake.

1.8 Malikale na Burudani

Maeneo ya malikale yakiendelezwa na kuhifadhiwa ipasavyo, hutumika kama sehemu muhimu ya burudani. Mara nyingi watu watembeleapo sehemu za malikale hawafuati tu kuelimika juu ya mambo watakayoyakuta hapo, bali hupumzisha akili zao kwa kushangaa na kushangilia maajabu ya kisayansi na kiteknolojia, au pengine kusikitika juu ya uduni wa mambo yalivyokuwepo zama hizo. Watu hufurahi kuona malikale zenye uhusiano na historia ya jamii mbalimbali, kama vile maendeleo ya teknolojia, mabadiliko ya sura ya nchi na viumbe.

1.9 Malikale na Mazingira

Malikale ni sehemu ya mazingira kiasi kwamba mara nyingi ni vigumu kutenganisha suala la uhifadhi wa malikale na utunzaji wa mazingira. Malikale ni chimbuko na kielelezo muhimu cha mahusiano kati ya mwanadamu na mazingira yake. Kwa hiyo uhifadhi endelevu wa malikale unachangia katika kulinda na kuhifadhi mazingira. Yapo maeneo mbalimbali ambayo kutokana na umuhimu wake kijamii yametumika kama maeneo ya ibada, au matambiko na hivyo kusababisha yaheshimiwe na kutunzwa. Mifano mizuri ni misitu na mapango ambayo katika baadhi ya maeneo yameweza kuepushwa na uharibifu wa binadamu kutokana na umuhimu wake kiutamaduni.

SURA YA PILI

2.0 HALI HALISI YA MALIKALE

2.1 Utafiti wa Malikale

Ingawa malikale huweza kupatikana kwa njia mbalimbali kama vile kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, kuokota, kununua na kuzawadiwa, njia ya kawaida na ambayo hutumika zaidi ni ya kufanya utafiti. Ieleweke kuwa hata kabla ya kuanza kwa tafiti zilizoletwa na wageni kutoka Ulaya, wahenga wetu walikuwa wakifanya utafiti kwa malengo ya kuvitambua vitu mbalimbali vya jadi katika mazingira yao.

Kwa hapa Tanzania, utafiti wa kisayansi uliowahusisha wageni katika fani ya malikale ulianza mwaka 1913 wakati Profesa Mjerumani aitwaye Hans Reck alipoongoza kundi la wataalamu wa miamba na malikale kwenye Bonde la Oldupai, lililopo Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha kufuatilia ugunduzi wa kibahati wa visukuku vya mifupa na zana za mawe uliofanywa na mtaalamu wa wadudu, Profesa Wilhelm Kettwinkel, Mjerumani pia, katika bonde hilo mwaka 1911.

Kuanzia miaka ya 1930, tafiti nyingi za kisayansi zimefanyika ambazo zimeibaini Tanzania kuwa miongoni mwa nchi mashuhuri duniani kwa kuwa na hazina kubwa ya malikale. Miongoni mwa hizo ni visukuku vya dinasoria wa jamii ya Branchysaurus vilivyogunduliwa na mhandisi, B. Saltler, kule Tendaguru, Lindi mwanzoni mwa karne ya ishirini; fuvu la zamadamu aliyeishi miaka milioni 1.75 iliyopita, aitwaye kitaalamu Australopithecus boisei, lililogunduliwa na Dkt. Mary Leakey na mumewe Dkt. Louis Leakey mwaka 1959; na

nyayo za zamadamu wengine wa spishi ya Australopithecus afarensis, pamoja na za wanyama na ndege mbalimbali walioishi miaka milioni 3.6 iliyopita zilizogunduliwa na Dkt. Mary Leakey mwaka 1976 katika Bonde la Oldupai na Laetoli, Arusha.

Tafiti nyingine ni za michoro ya miambani inayopatikana sehemu nyingi nchini, na hasa wilaya za Kondoa, Dodoma Vijijini, Singida Vijijini, Iramba, Bukoba Vijijini na Muleba; magofu ya majumba na makaburi yaliyojengwa kwa matumbawe kuanzia miaka mia nane iliyopita katika sehemu kadhaa za pwani, kama vile Tongoni, Wilaya ya Pangani, Mkoa wa Tanga; Kaole, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani; Kunduchi, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es salaam; Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, Wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi; Kimondo, kilichopo eneo la Ndolezi, Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Mbeya; visukuku vya kilimo cha umwagiliaji cha miaka zaidi ya mia tatu iliyopita vilivyopo Engaruka, Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha, na mengineyo mengi.

Kwa muda mrefu utafiti wa malikale hapa nchini ulikuwa unafanywa na wageni kwa vile wataalamu wazalendo walikuwa wachache sana, na karibu wote walikuwa wameajiriwa kama watawala wa taasisi za malikale na hivyo kukosa nafasi ya kufanya utafiti. Kasi kubwa ya utafiti wa wazalendo imejitokeza hasa baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanza kufundisha masomo ya akiolojia katika ngazi ya shahada mwaka 1985, hatua ambayo imeongeza idadi ya wataalamu wazalendo katika sekta ya malikale. Hata hivyo kuna sehemu nyingi ambazo bado hazijafikiwa na watafiti.

2.2 Uhifadhi wa Malikale

Malikale zikiishagunduliwa na kufanyiwa uchunguzi wa

kisayansi huhifadhiwa kwa nia ya kuweka kumbukumbu na hata kwa ajili ya kutoa nafasi ya kurudia uchunguzi kwa baadaye kulingana na mabadiliko ya nadharia, mbinu na teknolojia.

Historia ya uhifadhi wa malikale kisheria inaanzia mwaka 1937 ilipoanzishwa Sheria ya Uhifadhi wa Majengo ya Kihistoria. Mwaka huo pia ulishuhudia kuanzishwa kwa Makumbusho ya Kumbukumbu ya Mfalme George V. Idara ya Mambo ya Kale ilianzishwa rasmi mwaka 1957. Wakati huo Idara ilijihusisha zaidi na kutafuta na kuorodhesha sehemu zilizokuwa na kumbukumbu za kihistoria, hususan sehemu ya mwambao.

Mwaka 1962 yalitokea mabadiliko mawili muhimu katika sekta ya urithi wa utamaduni. Kwanza kuliundwa wizara ya kushughulikia masuala haya ambayo iliitwa Wizara ya Utamaduni na Vijana. Pili, Makumbusho ya Kumbukumbu ya Mfalme George V yalibadilishwa na kuitwa Makumbusho ya Taifa. Miaka miwili baadaye, 1964, ilipitishwa Sheria ya Mambo ya Kale Cap. 330. Sheria hii ambayo ilifanyiwa marekebisho makubwa mara ya mwisho mwaka 1979, ndiyo inayoongoza shughuli zote za utafiti, uhifadhi, utunzaji na uendeshaji wa malikale hapa nchini hadi leo.

Katika kipindi hiki chote, sekta ya malikale imepata mafanikio mengi. Licha ya kuimarisha utafiti, serikali kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa imeweza kuratibu na kuhifadhi maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kukarabati baadhi ya majengo ya Kihistoria kama vile maboma ya Wajerumani ya Mikindani Mkoani Mtwara na Mahenge Mkoani Morogoro; Hospitali ya Ocean Road, Dar es Salaam na baadhi ya majengo ya kihistoria kama vile Jengo la Ikulu, Dar es Salaam na majengo yaliyopo katika mji wa Bagamoyo. Maeneo mengine

yaliyohifadhiwa ni pamoja na eneo ia Bonde la Olduvai mkoani Arusha na sehemu yenye visukuku vya nyayo Laetoli, Michoro ya miambani wilayani Kondoa na Singida Vijijini, na Mapango ya Amboni, Tanga.

Idara pia imefanikiwa kuandikisha magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na michoro ya miambani ya Kondoa-Irangi kwenye orodha ya urithi wa utamaduni wa Dunia chini ya mpango wa Shirika la Kielimu, Kisayansi na Kiutamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO); imeanzisha makumbusho vituoni Kaole; Oldupai; Ujiji, na Kalenga. Halikadhalika, vituo vya kumbukumbu na taarifa vimeanzishwa katika baadhi ya sehemu kama Isimila; Kondoa na Bagamoyo.

Pamoja na juhudi za uhifadhi zilizofanywa hadi sasa, sekta hii bado inakabiliwa na matatizo mbalimbali, ambayo kwa kiasi kikubwa, huchangiwa na ukosefu wa sera pamoja na wananchi kuwa na uelewa mdogo kuhusu maana na umuhimu wa malikale na uhifadhi wake. Kasoro hii imesababisha, kwa mfano, uharibifu na wizi unaohusisha kubomoa majengo ya kale ili kupata mawe kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kisasa; kubomoa majengo na makaburi ya kihistoria ili kupata nafasi ya ujenzi wa nyumba za kisasa; na kubadilisha sura na usanifu wa asili wa majengo ya kihistoria kwa kutumia teknolojia za kisasa na hivyo kupoteza uasili wake. Kumekuwa pia na uharibifu katika michoro ya miambani kwa kuandika au kuigiza picha ama maandiko kwa kutumia kalamu, mkaa, masizi ama chaki. Mbali ya uharibifu unaofanywa na binadamu, upo mwingine unaosababishwa na nguvu za asili kama vile jua, mvua, mmomonyoko wa ardhi, ukame na upepo.

Licha ya kuwepo Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964,

uhifadhi wa malikale umekuwa ukipwaya kutokana na kukosekana kwa sera katika sekta hii ambayo ingetoa dira na kipimo katika kuhifadhi na kuendeleza rasilimali hizo.

SURA YA TATU

3.0 UMUHIMU NA MALENGO YA SERA

3.1 Umuhimu wa Sera ya Malikale

Sekta ya malikale inalo jukumu la kuhifadhi na kuendeleza malikale za nchi. Hili ni jukumu kubwa na muhimu na hivyo linahitaji utaratibu madhubuti unaoonyesha tulikotoka, hapa tulipo, na tunakoelekea. Katika miaka ya karibuni kumetokea mabadiliko mengi hapa nchini na nje ya nchi katika nyanja za teknolojia, uchumi, jamii, siasa na mazingira. Mabadiliko haya yanaweza kuyumbisha uendeshaji wa sekta kama hakuna dira madhubuti inayotoa msimamo wa uelekeo.

Ingawa baadhi ya maelekezo ya kitaifa kuhusu uhifadhi wa urithi wa utamaduni yanapatikana katika Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 na katika Sera ya Utalii ya mwaka 1999, Sera hizo zinagusa vipengele vichache tu vihusuvyo malikale. Hivyo basi iko haja ya kuwa na sera maalumu ya malikale yenye kuainisha mambo muhimu ya kutekeleza katika uhifadhi na kutoa mwongozo na kuelekeza namna ya kusimamia masuala yale yahusuyo malikale pekee.

3.2 Malengo ya Sera ya Malikale

Lengo la jumla la Sera ya Malikale ni kuboresha mchango wa Sekta ya Malikale katika kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za utamaduni ikiwa ni pamoja na kuendeleza utalii wa urithi wa utamaduni kwa ajili ya ustawi wa taifa na manufaa ya binadamu wote.

Malengo mahususi ya Sera ya Malikale ni:

- Kufafanua dhima na majukumu ya jamii, watu binafsi, mashirika, na asasi mbalimbali zinazosimamia malikale;
- Kuainisha jinsi shughuli za malikale zitakavyoendeshwa na kusimamiwa;
- Kuweka ufafanuzi stahili wa kulinda, kusimamia, kutunza, kuhifadhi, kuendesha na kuendeleza malikale na urithi wa utamaduni kwa ujumla, na
- Kuainisha namna bora ya kusimamia utafiti na uhifadhi wa malikale kwa kufafanua jinsi wadau mbalimbali ikiwemo serikali na taasisi zake, sekta binafsi na umma kwa ujumla watakavyojihusisha katika shughuli za uhifadhi na uendelezaji wa malikale.

SURA YA NNE

4.0 HOJA NA MATAMKO YA SERA

4.1 Utafiti

Utafiti ni muhimu ili kuweza kujua aina ya malikale, ubora wake na eneo inapopatikana. Taarifa hizi husaidia katika kupanga mipango endelevu ya sekta ya Malikale. Tafiti za malikale nyingi zimefanywa katika maeneo fulani fulani tu, chache zimefanywa na wazalendo na nyingi watafiti toka nje ya nchi wakiwa wenyewe au kwa kushirikiana na watafiti wazalendo. Tafiti hizi kwa mfano, zilizofanywa Olduvai, zimeliletea taifa kujulikana ndani na nje ya nchi.

Hakuna mwongozo wa kitaifa unaotoa kipaumbele cha maeneo na mada za utafiti. Hii inachangia kutokuwepo kwa taarifa za maeneo mengine na kusababisha watafiti wawe wanafanya tafiti juu ya mada na mahali wanapoona panakidhi malengo yao.

Nchi yetu pia haina maabara bora na za kisasa za kufanyia uchambuzi wa masalia mbalimbali kama vile mawe, metali, mimea, makombe na mifupa. Tatizo hili huchelewesha upatikanaji wa matokeo ya utafiti kwani watafiti hulazimika kusafirisha nje ya nchi malikale wanazopata katika tafiti zao ili kufanya uchunguzi wa kina. Licha ya kuongeza gharama za utafiti, usafirishaji wa malikale zetu nje ya nchi unatoa mwanya wa uharibifu na upoteaji wa mali hizo kwa watafiti wasiowaaminifu. Watafiti wazalendo, hawatoshelezi kiidadi na kitaaluma kulingana na mahitaji ya nchi.

Ili kuondoa upungufu huu, kuna umuhimu wa kuandaa

orodha ya sehemu zenye malikale kwa nchi nzima na kwa kutumia orodha hii, kuandaa utaratibu wa kipaumbele katika mada na maeneo ya utafiti vitakavyotumika kuwaongoza watafiti. Orodha na mada za kipaumbele itatakiwa kuboreshwa mara kwa mara. Kadhalika, utoaji wa vibali usizingatie uwezo wa kitaaluma pekee bali ujali pia maadili ya fani husika ili kuzuia uharibifu wa rasilimali zetu. Maabara za kisasa zianzishwe ili kuwawezesha watafiti wa malikale kufanya uchunguzi na uchambuzi wa kimaabara hapa hapa nchini.

Watafiti wanalo jukumu la kuwashirikisha wananchi katika utafiti na baada ya utafiti kurudisha taarifa za matokeo ya tafiti hizo kwa wananchi. Pia, ipo haja ya kuandaa mkakati wa namna ya kutunza na kutumia malikale katika utoaji wa elimu kwa jamii ili iweze kunufaika na tafiti hizo.

Matamko ya Sera kuhusu Utafiti

4.1.1. Shughuli zote za utafiti, ikiwa ni pamoja na utoaji wa vibali na kuweka mwongozo wa kitaifa kuhusiana na mahitaji ya taifa kimaada na kwa maeneo ya kufanyia utafiti, zitaratibiwa na kusimamiwa na taasisi husika.

4.1.2. Maadili ya utafiti wa malikale yatawekwa bayana katika sheria za malikale ili kuzuia uharibifu unaoweza kufanywa na watafiti au wadau wengine.

4.1.3. Majukumu ya watafiti na wajibu wao vitawekwa bayana ili kuhakikisha kwamba malikale zinazowekwa katika dhamana yao ikiwa ni pamoja na zile wanazozipeleka nje ya nchi kwa uchunguzi zinatunzwa vizuri na hatimaye kurejeshwa nchini kulingana na sheria na taratibu zitakazotajwa katika

vibali vya watafiti hao.

4.1.4. Uhamasishaji kuhusu uanzishwaji wa maabara za kisasa zitakazoweza kukidhi mahitaji ya msingi ya watafiti ili kupunguza utegemezi wa maabara za nje utafanyika.

4.1.5. Wadau watahamasishwa kufanya utafiti juu ya teknolojia za jadi ili kubaini mbinu zinazotumika ambazo zikiboreshwa zinaweza kuchangia katika tafiti za kisasa.

4.1.6. Orodha ya kudumu ya maeneo ya malikale nchini itaandaliwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa orodha hiyo inaboreshwa kila wakati.

4.1.7. Utafiti wa urithi wa utamaduni usioshikika, ikiwa ni pamoja na lugha za jadi, utapewa kipaumbele ili kupanua wigo wa utajiri wetu wa malikale.

4.2 Uhifadhi

Malikale ni sehemu ya mazingira ambayo inaweza kuathiriwa kwa namna mbalimbali na nguvu za asili kama vile mvua, unyevunyevu, joto, baridi, mmonyoko wa ardhi au nguvu za kijiolojia. Malikale huweza kuharibika kutokana na kuhamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu mbalimbali. Hivyo, uhifadhi wa malikale ni muhimu ili kuhakikisha kwamba maeneo yenye malikale kama makumbusho na malikale yenyewe yanadumu na kuendelezwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Historia ya nchi yetu inaonesha kuwa kabla na baada ya uhuru umekuwepo utaratibu kwa kupitia sheria ya mambo ya kale,

baadhi ya miji mikongwe na majengo hususan yale yenye kubeba sifa mbalimbali za kiusanifu, kiufundi, kisiasa na kiutamaduni yameainishwa na kutamkwa kuwa urithi wa taifa kupitia tangazo kwenye Gazeti la Serikali ili sifa za miji na majenzi hayo zibaki kuwa ushahidi wa historia, ustaarabu, ustadi na umahiri wa vizazi vilivyotangulia. Baadhi ya majengo yamekarabatiwa na sasa yanatumika kwa madhumuni mbalimbali.

Juhudi zimefanywa na serikali kuhakikisha elimu ya jumla ya malikale inatolewa kwa kiwango cha cheti, stashahada na shahada katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mikakati ya kushirikisha wadau katika uhifadhi endelevu wa malikale ikiwa ni pamoja na kuweka miongozo stahili ya kuzingatiwa vimeandaliwa na kusambazwa.

Hata hivyo, licha ya juhudi zinazofanyika, uhifadhi wa malikale unazingatia zaidi urithi unaoshikika kama vile magofu ya kihistoria na zana mbalimbali kuliko urithi usioshikika ikiwa ni pamoja na mila na desturi za jadi, lugha za asili na hadithi. Malikale yanayokusanywa na watafiti hayahifadhiwi katika maeneo yanapopatikana badala yake, baadhi hususan yale yanayohamishika na yenye umuhimu zaidi, huhamishwa na kuhifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa la Tanzania. Hii imesababishwa na ukweli kwamba mpaka sasa hivi hakuna maghala ya kuhifadhia mikusanyo vituoni. Licha ya maelekezo ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, shughuli za miradi mikubwa ya maendeleo zinafanyika bila kufanyika tathmini ya athari za miradi hiyo kwa malikale na wananchi wengi bado hawajatambua umuhimu na wajibu wao katika uhifadhi wa malikale ya nchi yetu kama utambulisho wao.

Ili kuondoa upungufu huu kuna haja ya kuhakikisha kuwa urithi wa utamaduni usioshikika unapewa umuhimu katika uhifadhi sambamba na urithi unaoshikika ili kuleta uwiano halisi wa urithi wetu wa utamaduni. Ili kuwawezesha watafiti na jamii kufanya kazi pamoja na hivyo kuwezesha kukuza ufahamu wa malikale zipatikanazo nchini malikale zinazokusanywa na watafiti hazina budi kuhifadhiwa na kufanyiwa uchambuzi katika maeneo zinapopatikana. Mitaala ya elimu na mafunzo nchini haina budi kuzingatia uhifadhi wa malikale. Vile vile, msisitizo katika tathmini ya athari za miradi mikubwa kwa malikale hauna budi kuwekwa ili kuzuia uharibifu wa urithi wetu wa utamaduni.

Matamko ya Sera kuhusu Uhifadhi

4.2.1 Shughuli zote za uhifadhi wa malikale, ikiwa ni pamoja na kuandaa sheria na kanuni zitakazoongoza wadau mbalimbali katika kuendesha shughuli za uhifadhi, zitaratibiwa na kusimamiwa na taasisi husika.

4.2.2 Mipango mahsusi ya uhifadhi endelevu wa miji na majengo ya kihistoria pamoja na maeneo mengine ya malikale itaandaliwa ili kuhakikisha kuwa urithi huu unadumu na unakuwa na manufaa kwa jamii yote.

4.2.3 Utaratibu wa kuingiza elimu na mafunzo ya uhifadhi endelevu wa malikale nchini kwenye mitaala ya shule na vyuo utawekwa.

4.2.4 Utaratibu utaandaliwa ili kuhakikisha kuwa malikale zinazokusanywa na watafiti zinahifadhiwa katika maeneo na vituo ambapo masalia hayo hupatikana na

pale itakapobidi yale tu yenye umuhimu zaidi yatahifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa.

4.2.5 Utaratibu utakaohakikisha kuwa miradi yote mikubwa inayohusu uchimbaji au utibuaji wa ardhi inatanguliwa na tathmini ya athari za miradi hiyo kwa malikale utawekwa bayana na gharama za kufanya tathmini hiyo zitakuwa ni sehemu ya mradi husika.

4.2.6 Wananchi watahamasihwa kutambua, kuthamini, kulinda na kuendeleza urithi wetu wa utamaduni kwa kupitia vyombo vya serikali, Taasisi za umma na za watu binafsi.

4.3 Kumbukumbu

Nchi yetu inazo kumbukumbu nyingi za Malikale zenye sifa kitaifa na kimataifa ambazo baadhi zimeitangaza nchi nje ya mipaka yake. Utunzaji sahihi wa kumbukumbu huwezesha kupima ufanisi na kutoa tathmini ya utekelezaji wa majukumu.

Kumbukumbu zilzopo hapa nchini zimetunzwa katika Makumbusho ya Taifa la Tanzania, Maktaba ya Taifa, kwenye vituo vya kumbukumbu na taarifa na vituo vya mambo ya kale. Kumbukumbu nyingi ziko mikononi mwa watu.

.

Hata hivyo, pamekuwepo na upungufu katika kuorodhesha, kutunza na kusambaza taarifa zinazohusu maeneo ya Malikale. Hakuna utaratibu mzuri wa kuorodhesha, kutunza, na kusambaza taarifa hizo. Katika kufanikisha azma hii, kuna umuhimu wa kutilia mkazo uanzishaji wa maktaba na vituo

vya kumbukumbu na taarifa katika maeneo yote muhimu ya malikale nchini; kuhamasisha umma kutambua, kuthamini na kutunza vielelezo vya malikale vilivyopo, kuwashawishi watu wanaotunza malikale kwenye maeneo wanayoishi ili watoe taarifa kwa mamlaka husika. Aidha, kumbukumbu muhimu za viongozi wa kitaifa na watu waliowahi kutoa mchango muhimu katika jamii, kama vile mashujaa wa vita, zinapaswa kuhifadhiwa.

Matamko ya Sera kuhusu Kumbukumbu

4.3.1. Uanzishaji wa vituo vya kumbukumbu na taarifa katika maeneo mbalimbali ya malikale, hususan, maeneo yenye masalia mengi au muhimu utahamasishwa.

4.3.2. Mashirika, Vikundi vya watu binafsi vinavyohifadhi malikale walizozirithi kimila au kuzipata kwa njia nyingine watahamasishwa kuanzisha Makumbusho au vituo vya Kumbukumbu na Taarifa kwa kuzingatia sheria, utaratibu na kanuni zilizopo.

4.3.3. Utaratibu wa kuhamisha umiliki wa malikale kutoka kwa watu binafsi au taasisi, ambazo zenyewe ama hazipendi ama hazina uwezo wa kuendelea kuzihifadhi, utaandaliwa.

4.3.4. Utunzaji wa kumbukumbu muhimu za viongozi na mashujaa wa kitaifa utaimarishwa.

4.4 Takwimu

Takwimu ni muhimu katika kupanga na kutekeleza malengo. Husaidia kupima mafanikio yanayopatikana baada ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuainisha matatizo na upungufu katika utekelezaji na kurahisisha upendekezaji wa hatua za kuchukua. Hivyo huwezesha uandaaji wa bajeti halisi kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, idara imejiwekea mbinu mbali mbali zinazowezesha ukusanyaji wa tawimu hususan zinazohusu utafiti, uhifadhi wa maeneo na ukarabati wa majengo, wageni mbalimbali watembeleao vituo vya malikale na mapato. Kupitia takwimu hizi, idara imekuwa na utaratibu wa kuainisha maeneo ya kipaumbele kwa kipindi cha miaka mitatu na kuweka mikakati ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa rasilimali watu, vitendea kazi na fedha kupitia serikali na wafadhili. Idara pia imeweza kuainisha maeneo ya kushirikisha wadau kwa shughuli za kibiashara kwa lengo la kutumia vituo na maeneo ya malikale kama vyanzo vya mapato na hivyo kupunguza umasikini miongoni mwa jamii. Hivi sasa kuna ongezeko kubwa la jamii kupitia vikundi vya kiserikali na visivyo vya kiserikali wanaojihusisha na utalii wa urithi wa utamaduni nchini. Jamii hii ni fursa stahili katika ukusanyaji wa takwimu.

Hata hivyo pamoja na mafanikio hayo, takwimu nyingi ziko mikononi mwa wanaozikusanya. Idara haina mfumo stahili wa ukusanyaji wa takwimu hivyo ni vigumu kujua kwa uhakika ni watalii wangapi wanaotembelea malikale nchini kwa lengo la utalii wa utamaduni na mapato yanayotokana nao. Vilevile ni vigumu kufuatilia viwango vya ubora na uharibifu wa malikale kuanzia ngazi za vijiji, wilaya, mikoa hadi taifa kutokana na

kutokuwepo kwa muundo unaowezesha nguvukazi ya ukusanyaji wa takwimu zihusianazo na malikale.

Kuna haja ya kuimarisha ushirikiano na wadau wote wa malikale nchini ili kurahisisha uainishaji maeneo yote yenye takwimu zihusuzo malikale na uandaaji wa mfumo sahihi.

Matamko ya Sera kuhusu Takwimu

4.4.1. Ukusanyaji na utunzaji wa takwimu sahihi za malikale kwa kutumia mbinu na teknolojia stahili ili kufanikisha utekelezaji wa malengo ya sekta hii utaratibiwa na kusimamiwa na taasisi husika;

4.5 Ushirikishwaji wa wadau

Malikale ni utambulisho wa taifa, hivyo jukumu la uhifadhi wake ni la umma mzima. Jamii ina haki ya kuelimishwa na kushirikishwa kutambua umuhimu wa malikale ya nchi kwa vile malikale nyingi ziko mikononi mwa jamii yenyewe. Kwa kuzingatia ukweli huu, serikali kwa kipindi chote inafanya kazi na jamii kwa kutoa miongozo ya kuzingatiwa kuhakikisha kuwa malikale ya nchi haiharibiwi wala kupotea. Miongozo pia imewekwa kuhakikisha kuwa utekelezaji wa kazi zote zinazohusu malikale unapata ridhaa ya wamiliki na kutambuliwa na uongozi wa serikali eneo lilipo kuanzia ngazi ya kijiji hadi mkoa.

Wananchi wamekuwa wakichangia katika utoaji wa taarifa kwa watafiti wa malikale na kushiriki katika utekelezaji kwa viwango tofauti tofauti jambo ambalo limeiwezesha Tanzania kuwa na mchango mkubwa katika kukua kwa sayansi ya malikale duniani. Katika kuchangia huduma za maendeleo

katika baadhi ya vijiji, baadhi ya wanajamii wanatoa huduma ya ulinzi wa hiari wa malikale iliyoko katika maeneo yao na hivyo kupunguza uharibifu kwa kuzingatia miongozo inayotoa maelekezo ya namna bora ya kushirikisha jamii.

Ushiriki wa Halmashauri za wilaya na jamii kwa ujumla katika uhifadhi na uendelezaji wa malikale bado haujawa na nguvu kubwa kwa sababu malikale haijatangazwa vya kutosha. Vyombo vya habari havijajihusisha ipasavyo katika kuhamasisha na kuelimisha jamii. Bado kuna dhana miongoni mwa jamii kuwa utafiti, uhifadhi na uendelezaji wa malikale ni jukumu la serikali. Mipaka ya uwajibikaji katika ngazi za vijiji, wilaya, mikoa na taifa na hata baina ya taaluma haijawekwa bayana wala kufahamika miongoni mwa jamii. Nafasi ya malikale katika ukuaji wa miji na taifa bado ni kitendawili.

Ni wajibu wa asasi na mashirika yanayohusika na malikale kuwajibika kuhamasisha na kuelimisha jamii ili kuboresha viwango vya ushiriki katika uendelezaji wa malikale nchini. Vyombo vya habari vikiwemo redio, magazeti na televisheni pamoja na sanaa vikitumiwa ipasavyo vina nafasi kubwa ya kuifanya jamii iwe na mchango wa kutegemewa katika uhifadhi wa malikale na uanzishaji wa makumbusho.

Matamko ya Sera kuhusu Ushirikishaji Wadau

4.5.1. Vikundi au vyombo mbalimbali katika jamii vitahamasishwa kuanzishwa ili kusimamia maeneo yaliyohifadhiwa mijini na vijijini na hivyo kusogeza shughuli za uhifadhi kwa wadau hao.

4.5.2. Haki na wajibu wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Wananchi katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na

kunufaika na rasilimali za malikale zitawekwa bayana.

4.5.3. Sekta binafsi na taasisi mbalimbali zitahamasishwa kuanzisha shughuli za makumbusho katika sehemu mbalimbali nchini.

4.6 Uwekezaji katika utalii wa utamaduni

Malikale hutoa mchango mkubwa katika uchumi ikitumiwa kama kivutio cha utalii na eneo la uwezekaji kwa kuzingatia misingi na kanuni za uhifadhi. Maeneo ya malikale kama vile kule Mikindani yamedhihirisha ukweli huu. Uwekezaji katika maeneo ya malikale unahitaji fedha nyingi kutokana na umuhimu na matakwa ya uhifadhi. Hivyo, iwe ni lengo la serikali kuandaa utaratibu bora wa uwekezaji na kuweka mazingira stahili ya kuboresha miundombinu kwa njia ya sekta binafsi au kupitia serikali yenyewe. Hii ni pamoja na kuhamasisha jamii, watu binafsi, mashirika na asasi mbalimbali kuwekeza katika sekta ya malikale ili kushirikisha umma, kujiongezea mapato na kupunguza mzigo wa gharama za uendeshaji. Aidha, serikali ina jukumu la kuchukua tahadhari dhidi ya athari za uwekezaji katika mazingira na rasilimali za utamaduni. Kwa mfano, kumekuwepo na mmomonyoko mkubwa wa urithi wa utamaduni utokanao na utekelezaji wa mipango na miradi mbalimbali ya maendeleo. Mmomonyoko wa namna hii umetokana na ukosefu wa Sera ambayo ingewataka na kuwabana watekelezaji wa miradi ya aina hii kufanya tathmini za athari za miradi hiyo kwa jamii zinazoizunguka na utamaduni wao kabla miradi hiyo haijatekelezwa.

Matamko ya Sera kuhusu Uwekezaji katika Utalii wa Utamaduni

4.5.4. Vikundi mbalimbali kama vile vijana, wanawake, walemavu, watu binafsi na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali wataelimishwa na kuhamasishwa ili watambue umuhimu wa kuendesha shughuli za utalii katika maeneo ya urithi wa utamaduni kama vile kuanzisha makumbusho, vituo vya utalii na maduka ya vitu vya utamaduni.

4.6.2 Uanzishaji na uendelezaji wa miradi ya maendeleo na tathmini ya athari za uendelezaji huo kwa jamii na utamaduni wao. Gharama za kufanya tathimini hiyo zitakuwa ni sehemu ya gharama za mradi husika.

4.7 Utaalamu, Mafunzo na Ajira

Ufanisi katika uhifadhi wa malikale unategemea sana ubora wa wataalamu, mazingira mazuri ya kazi na vitendeakazi. Kiutendaji, malikale inapatikana katika nchi nzima ya Tanzania. Aidha, kazi za uhifadhi wa malikale zinazingatia sana maadili yanayokubalika Kimataifa. Hivyo, ufanisi wa kazi hii unategemea taaluma stahili katika kusimamia, kuhifadhi, kuendeleza, kuendesha na kutangaza urithi huo.

Kwa mantiki hiyo, watalaam wa kutosha na wenye sifa zinazotakiwa kwa kazi hii wanahitajika sana. Hata hivyo, watalaam waliopo nchini ni wachache na hawakidhi mahitaji halisi ya uhifadhi. Hali hii imesababisha baadhi ya maeneo yenye urithi wa utamaduni kutokuwa na wasimamizi na watendaji.

Hivyo, idadi na ujuzi ni vitu muhimu vya kuzingatiwa katika ajira ya wafanyakazi wa sekta ya malikale. Mafunzo ya wafanyakazi hayana budi kuimarishwa ili kuwawezesha wale waliopo kazini waweze kupata ujuzi unaolingana na mabadiliko ya kiteknolojia. Ili hili lifanikiwe inatakiwa kuandaliwe utaratibu mahsusi na endelevu wa kutathmini mahitaji ya nguvukazi na kuweka mikakati ya mafunzo kwa watumishi. Kwa taaluma zile ambazo hazitolewi hapa nchini, watumishi wapatiwe fursa za kwenda kusoma nje ya nchi. Ni dhahiri kuwa, utumiaji wa baadhi ya vifaa huhitaji stadi maalum. Hivyo kuna haja ya kuweka mkakati wa kudumu wa mafunzo ya stadi za kazi ili kumudu mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia yanayotokea siku hadi siku.

Matamko ya Sera kuhusu Utaalamu, Mafunzo na Ajira

4.5.5. Mafunzo na ajira vitasimamiwa na taasisi husika ili kuhakikisha kuwa sekta ya malikale inajitosheleza kwa wataalam katika ngazi zote.

4.5.6. Uanzishwaji wa vyuo vya mafunzo ya fani ya uhifadhi wa malikale nchini utahamasishwa ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa wataalamu na kupunguza gharama ya kuwasomesha nje ya nchi.

4.5.7. Mafunzo katika nyanja zote za malikale yatapewa kipaumbele ili kujijengea uwezo wa kitaifa wa kiutafiti ili kuuelewa, kuulinda, kuuhifadhi na kuutangaza urithi wetu.

4.5.8. Elimu ya wafanyakazi na uongozi stahili vitaimarishwa ili kuwa na uendeshaji makini na utawala bora.

4.5.9. Pale ambapo wataalamu waajiriwa katika sekta ya malikale hawatoshi, ushirikiano na wataalamu washauri utatumika ili kuboresha huduma na majukumu mbalimbali.

4.8 Vitendea Kazi

Ili mtumishi aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa muda unaotakiwa, hana budi kuwa na vitendea kazi vinavyohitajika. Hivyo, utoshelevu na ubora wa vitendea kazi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha ufanisi wa kazi katika sekta yoyote.

Sekta ya Malikale imejitahidi kuboresha vitendea kazi kwa kuzingatia teknolojia ya kisasa katika baadhi ya nyanja. Pamoja na hayo, kuna upungufu wa vitendea kazi kama vile kompyuta zenye programu stahili, magari yenye kustahimili mazingira magumu ya maeneo ya utafiti, samani na ofisi zenye ubora kiuhifadhi.

Kwa kuzingatia umuhimu wa vitendea kazi, kuna haja ya kujenga tabia ya kukarabati au kubadilisha vitendea kazi vichakavu mara kwa mara. Aidha, kutokana na ukweli kwamba teknolojia ya kisasa inabadilika kwa kasi sana, upo umuhimu wa kujiandalia mikakati endelevu ya kuhakikisha kuwa kila inapowezekana vitendea kazi vinaendana na mabadiliko ya kiteknolojia.

Matamko ya Sera kuhusu Vitendea Kazi

4.5.10. Vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa vya ofisini, uhifadhi, maabara, usafiri na utafiti vitaimarishwa

ikiwa ni pamoja na utoaji wa mafunzo kwa watumiaji ili waweze kuvitumia ipasavyo na kwa ufanisi.

4.9 Maeneo ya Malikale

Maeneo ya malikale ni rasilimali za utamaduni, zinazoshikika na zisizoshikika; zinazohamishika, na zisizohamishika zilizo nchi kavu au majini zenye umri wa miaka mia moja (100) na kuendelea, au zile ambazo kutokana na umuhimu wake zimeainishwa na kutangazwa na Waziri mwenye dhamana kulingana na sheria na kanuni za serikali zinazosimamia malikale nchini.

Baadhi ya maeneo ya malikale yameorodheshwa na kutangazwa katika gazeti la serikali kama maeneo yanayohifadhiwa. Maeneo mengine hayapo chini ya umiliki wa Serikali. Hali hii inaleta utata kutokana na migongano ya nia, mipango na taratibu za kuyaendeleza kati ya Serikali yenye nia ya uhifadhi endelevu na wamiliki wenye kujiona huru kufanya wapendavyo katika maeneo hayo. Lakini, hata maeneo yanayomilikiwa na Serikali, ni machache sana yenye hatimiliki. Hali hii siyo nzuri kwa uhifadhi endelevu kwani kuna hatari ya kuzuka kwa utata wa umiliki kwa siku za usoni. Upungufu huu unapaswa kurekebishwa.

Kwa mantiki hiyo, serikali ina jukumu la kushirikisha jamii katika kubaini, kutambua na kuorodhesha maeneo yenye malikale ambayo hayajatangazwa ili yatangazwe.

Ni vema serikali ihakikishe malikale zinaainishwa kuwa miongoni mwa vivutio muhimu vya utalii. Nchi yetu ina jukumu la kukuza na kuendeleza utalii wa kiutamaduni ambao unaendelea kukua kwa kasi ulimwenguni kote. Aidha,

miundombinu, kama vile barabara, inatakiwa kuboreshwa ili kuhakikisha maeneo yenye malikale yanafikika kwa urahisi. Hata hivyo, kuna haja ya kuchukua hadhari dhidi ya athari za utalii kwa malikale kama vile ongezeko la kasi ya uchakavu wa urithi huu linalotokana na kugusa, kukanyaga, kuegemea au kuhamisha.

Matamko ya Sera kuhusu Maeneo ya Malikale

4.9.1. Malikale zitatambuliwa, kuorodheshwa na kutunzwa ili kuwa miongoni mwa vivutio muhimu vya utalii.

4.9.2. Maeneo ya wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afirika yatatambuliwa na kuhifadhiwa kwa kushirikiana na nchi husika.

4.9.3. Vitu vyote vilivyotengenezwa na binadamu vitatambuliwa, kisheria, kuwa ni kumbukumbu za taifa vinapofikisha umri wa miaka mia moja.

4.9.4. Maeneo yote muhimu ambayo hayajatangazwa katika gazeti la Serikali yatafanywa hivyo ili kutambua umuhimu wake na kuyatunza kulingana na sheria na kanuni husika.

4.9.5. Utaratibu utawekwa utakaohakikisha kuwa uendeshaji wa shughuli za utalii katika maeneo yenye malikale unafanyika bila kuathiri malikale hizo.

4.9.6. Mipaka ya maeneo yote yaliyotangazwa na yatakayotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa Kumbukumbu za Taifa itawekwa na hatimiliki kutolewa ili kuondoa utata na migongano ya taratibu

za kuyaendesha.

4.9.7. Miundombinu kama vile barabara, viwanja vya ndege, usafiri wa majini, umeme na nyinginezo kwenye sehemu muhimu za malikale itaboreshwa ili kuhakikisha maeneo hayo yanafikika kwa urahisi kwa manufaa endelevu ya sehemu hizo

4.10 Ushirikiano wa Kimataifa

Shughuli nyingi za uhifadhi, uendelezaji na uendeshaji wa malikale katika nchi yoyote zinahitaji sana suala zima la ushirikiano wa kimataifa. Mathalani, biashara ya malikale ambayo huchangia sana katika kuzidisha wizi wa mali hizi ni ya kimataifa kiasi kwamba siyo rahisi nchi moja peke yake kuweza kupambana na wizi huo. Hata hivyo, mahusiano mazuri kati yetu na mashirika ya kimataifa kama vile UNESCO, ICCROM, ICOMOS, ICMAH, ICOM na mengineyo mengi yamesaidia sana kupata ushauri muhimu ikiwa ni pamoja na kutuwezesha kusimamia mikataba ya kimataifa ya uhifadhi wa rasilimali zenye hadhi ya kimataifa yaani Urithi wa Utamaduni wa Dunia. Mashirika haya yanayo nafasi kubwa katika kushauri na kusimamia mikataba ya kimataifa na kushirikiana na serikali, jamii na taasisi au asasi mbalimbali katika kuendeleza uhifadhi wa maeneo yenye rasilimali za urithi wa utamaduni wenye viwango vya kitaifa na kimataifa. Vilevile, serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa malikale zote zilizoko nje ya nchi zinarejeshwa.

Hivyo kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba ushirikiano kati ya asasi zinazosimamia rasilimali za utamaduni nchini na asasi nyingine za kimataifa unadumishwa. Ushirikiano wa

kimataifa pia unasaidia kupunguza tatizo sugu la biashara haramu ya malikale ambalo limeenea ulimwenguni kote na kusaidia malikale zetu zilizopelekwa nje ya nchi kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wizi, kurejeshwa kwa urahisi.

Matamko ya Sera kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa

4.10.1. Ushirikiano wa Kimataifa utasimamiwa, kuendelezwa, kudumishwa na kuhimizwa ili kubadilishana uzoefu.

4.10.2. Mikataba ya kimataifa, yenye manufaa kitaifa katika uhifadhi wa urithi wa utamaduni wa nchi, itaridhiwa ili kuwezesha vita dhidi ya biashara haramu ya malikale na urejeshwaji wa malikale za taifa zilizoko nje ya nchi.

SURA YA TANO

5.0 MASUALA MTAMBUKA YA SERA

Suala la uhifadhi na uendelezaji wa malikale linahusisha sekta mbalimbali katika jamii. Hivyo, utekelezaji wa Sera hii hauna budi kushirikisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Sekta Binafsi, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na Mawakala wa Serikali na vyombo vingine vya dola. Majukumu ya Taasisi hizi yatakuwa kama ifuatavyo:-

5.1 Serikali Kuu

Katika usimamizi na uendeshaji wa malikale, Serikali Kuu itatekeleza majukumu yafuatayo:

- Kulinda, kuhifadhi na kuendeleza majengo na maeneo ya kihistoria ya Malikale yanayojumuisha urithi wa utamaduni unaoshikika na usioshikika kwa mujibu wa sheria za Mambo ya Kale;

- Kusimamia sheria ya Malikale ili kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji kwa kufanya marekebisho inapobidi ili kuendana na mahitaji ya kusimamia, kulinda, kuhifadhi, kutafiti na kuendeleza urithi wa utamaduni;

- Kuratibu, kusimamia na kutoa vibali vya tafiti mbalimbali nchini katika nyanja za akiolojia, palaentolojia, ikiwa ni pamoja na vibali vya kupiga picha na kusafirisha mikusanyo ya urithi wa utamaduni nje ya nchi kwa lengo la uchunguzi zaidi ;

- Kufanya utafiti wa Malikale Tanzania Bara kwa kushirikiana na watafiti ndani na nje ya nchi ;

- Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Mambo ya Kale kwa lengo la kushirikisha umma katika kuhifadhi na kuendeleza urithi huo ;

- Kutoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi, asasi au watu binafsi kuhusu uhifadhi, ukarabati na uboreshaji wa majengo na maeneo ya kihistoria ;

- Kushiriki kikamilifu katika mikataba ya kimataifa ambayo nchi ni mwanachama ; na

- Kuweka kumbukumbu sahihi kitaifa, kiwilaya, kitarafa, na kivijiji ya jumla ya maeneo ya Malikale na pia kuweka kumbukumbu ya maeneo ambayo hayajafanyiwa utafiti.

5.2 Serikali za Mitaa

Kwa kuzingatia mgawanyo wa madaraka kutoka serikali kuu hadi serikali za mitaa, majukumu ya usimamizi ya serikali za mitaa katika sekta ya Malikale yamepanuliwa katika upeo na uzito wake. Katika mfumo huu, serikali za mitaa zitawajibika kama ifuatavyo:-

- Kutunga sheria ndogondogo na kushiriki katika utungaji wa kanuni;

- Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi malikale;

- Kushiriki katika uhifadhi wa maeneo ya urithi wa utamaduni; na

- Kutambua na kupendekeza maeneo yenye hadhi ya kuhifadhiwa kwa ajili ya kutangazwa kama maeneo yanayohifadhiwa.

5.3 Jamii

Usimamizi wa rasilimali za urithi wa utamadunii kwa ajili ya matumizi endelevu unahitaji, miongoni mwa mambo mengine, kubadilisha mtazamo kuhusu desturi za matumizi ya rasilimali hizo. Hivyo, jamii ya watumiaji ambao wanajihusisha na rasilimali siku hadi siku inapaswa kuhamasishwa na kuwezeshwa kutambua nafasi hiyo na kusaidiwa kuwajibika katika uhifadhi wa malikale. Kwa hiyo wajibu wao utakuwa kama ifuatavyo:-

- Usimamizi, utumiaji na uendelezaji wa rasilimali za urithi wa utamaduni na kujipatia ajira kupitia urithi huo;

- Kushiriki katika kutunga sheria ndogondogo na kusimamia utekelezaji wake;

- Uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali zinazotokana na urithi wa utamaduni; na

- Kushiriki katika usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za urithi wa utamaduni.

5.4 Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali

Ili kuongeza uwezo na kukuza maendeleo endelevu ya Sekta ya Malikale, mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ni muhimu kama kichocheo katika utekelezaji wa maamuzi ya uongozi na uandaaji wa Sera ya Malikale. Kwa hiyo, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali yatashiriki kama ifuatavyo:-

- Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani;
- Kujenga uwezo wa uendeshaji;
- Kutoa mafunzo na misaada ya kiufundi;
- Kugharimia shughuli za malikale na mazingira; na
- Kukuza dhima za kijinsia na kuzipa uwezo jamii.

5.5 Sekta binafsi

Sekta binafsi zitaongeza uwekezaji, kuboresha shughuli na usimamizi wa jumla katika urithi wa utamaduni na kuzidisha ugharimiaji wa shughuli na mauzo ya bidhaa za malikale. Kwa hiyo, sekta binafasi itashiriki kama ifuatavyo:-

- Kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali za urithi wa utamaduni;
- Kuwezesha au kugharimia uwekezaji katika sekta ya Malikale;
- Kuzalisha bidhaa za urithi wa utamaduni;

- Kutafuta masoko ya bidhaa za urithi wa utamaduni;

- Kutumia mwongozo na kanuni katika usimamizi wa urithi wa utamaduni;
- Kuzingatia tathmini ya athari za mazingira katika uwekezaji kwenye sekta ya malikale;

- Kushiriki katika uhifadhi, uendelezaji, usimamizi na matumizi endelevu ya urithi wa utamaduni;

- Kuhamasisha na kutoa huduma za ugani; na

- Kuendeleza utalii wa urithi wa utamaduni kwa kutoa ajira, zana za urithi wa utamaduni na huduma.

5.6 Jumuiya za Kikanda na Kimataifa

Hawa ni wabia katika maendeleo ya kudumu. Kwa hiyo, ushiriki wao utakuwa kama ifuatavyo:-

- Kutoa misaada ya kifedha;

- Kujenga uwezo wa uendeshaji kwa njia ya misaada ya kiufundi; mafunzo, utafiti na ubadilishaji wa uzoefu; na

- Kuwezesha utekelezaji wa majukumu na mikataba ya Kimataifa.

5.7 Mawakala wa Serikali na vyombo vingine vya dola

Hawa watasaidia katika usimamizi wa uendeshaji wa malikale na uhifadhi wa mazingira.

SURA YA SITA

6.0 MUUNDO WA KITAASISI NA KISHERIA

6.1 Muundo wa Kitaasisi

Tangu kuanzishwa kwa Idara ya Mambo ya Kale mwaka 1956, utaratibu umekuwepo kuhakikisha majukumu yanatekelezwa ipasavyo kwa kuzingatia utaalam, ujuzi na uzoefu wa kazi.

Baada ya uhuru mwaka 1961 hadi mwaka 1993 muundo ulikuwa na Mkurugenzi, Wahifadhi, Wahifadhi Wasaidizi na Mafundi. Kiutendeji, Idara imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni Sehemu ya Kumbukumbu, Maktaba na Mafunzo; Sehemu ya Utafiti na Maabara na Sehemu ya Uhifadhi, Takwimu na Elimu kwa Umma. Muundo uliofuata baada ya mwaka 1993, uliondoa kada ya wahifadhi wasaidizi/mafundi wahifadhi wasaidizi.

Muundo unaoandaliwa ili kutekeleza Sera ya Malikale unalenga kuweka mgawanyo wa majukumu kuwa na Mkurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi watatu, Wahifadhi Mambo ya Kale, Wahifadhi Mambo ya Kale Wasaidizi, Mafundi Wahifadhi Mambo ya Kale na Mafundi Wahifadhi Mambo ya Kale Wasaidizi.

6.2 Muundo wa kisheria

Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 1979, kanuni, notisi na amri zake ndicho chombo kikuu cha kisheria katika usimamizi wa sera

hii ya Malikale. Vyombo vingine ni Katiba ya nchi ya mwaka 1994 (kifungu namba 9 (c)), Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 (Kifungu S.1.), sheria ya Makumbusho namba 7 ya mwaka 1980 na sheria ya mazingira ya mwaka 2004. Idadi kubwa ya sheria hizi zinahitaji kupitiwa, na sheria ndogo kuongezwa mara kwa mara ili kukidhi mahitaji ya sera.

SURA YA SABA

7.0 MWISHO

Sera hii imetoa matamko yatakayowekewa mikakati endelevu ya kutafiti, kutambua, kulinda, kuhifadhi na kuendeleza malikale kwa kushirikisha jamii na wadau wengine katika mipango ya uhifadhi wa urithi wa utamaduni kwa ngazi mbalimbali za utendaji. Malikale tuliyonayo ni hazina ya kujivunia na ni utambulisho wa taifa letu. Aidha kuanzisha na kuboresha miundombinu, pamoja na kuendeleza nguvukazi ni muhimu katika kutangaza maeneo ya malikale kama vivutio vya utalii bila kuathiri uhifadhi kwa lengo la kuinua kipato na kupunguza umasikini.

Sera imetoa matamko ambayo yanalenga kutatua mapungufu mbalimbali katika kuhifadhi na kuthamini urithi wa utamaduni kama rasilimali muhimu inayopaswa kutunzwa na kulindwa. Utoaji wa elimu kwa umma juu ya uhifadhi wa malikale umetiliwa mkazo mkubwa katika sera hii kama njia mojawapo ya kuendeleza urithi huu muhimu. Wizara inayosimamia malikale itaendelea kuelimisha jamii, wizara na asasi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali juu ya umuhimu wa kuhifadhi na kuendeleza malikale zilizopo katika maeneo yao. Utumiaji wa teknolojia za jadi katika uhifadhi wa malikale pamoja na ushirikiano wa kimataifa utainua kiwango cha umakini na kupanua wigo katika kubuni mbinu mpya za kuendeleza, kuhifadhi na kutumia rasilimali hizo muhimu na adimu.

Kufanikiwa kwa mikakati na matamko ya Sera hii kutategemea sana ushirikiano wa karibu na mgawanyo wa majukumu kati ya serikali, wananchi na wadau mbalimbali. Wizara

inayosimamia malikale itaendelea kubeba wajibu wa kusimamia uhifadhi endelevu wa malikale na vituo vya kumbukumbu na taarifa na kuratibu sera zote zinazohusiana na uhifadhi wa malikale kwa kushirikiana na wizara zingine.